



Jarida la

SIHA NA MAENDELEO

UTAWALA BORA

www.sihadc.go.tz

Mwezi Juni 2023

Toleo la 4

Halmashauri ya Siha



Haliuzwi

MAPOKEZI YA MWENGE WA UHURU WILAYA YA SIHA TAREHE 26 JUNI,2023



Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe.Dkt. Christopher Timbuka (aliyevaa skafu kushoto) akikabidhiwa Mwenge wa Uhuru na Mkuu wa Wilaya ya Ha Mhe.Amiri Mkalipai siku ya jumatatu asubuhi eneo la mapokezi katika kijiji cha Munge Kata ya DonyoMurwak tarehe **26/6/2023**.



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa ndugu **Abdalla Shaib Kaim** (hapo juu) akifungua shule mpya ya Msingi na awali Munge Kata ya DonyoMurwak tarehe **26/6/2023**,shule hii imejengwa na Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa **shilingi milioni 250 na Michango na nguvu za Wananchi shilngi milioni 20.7**



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Mhe.Duncan Urassa akipokea Mwenge wa Uhuru katika eneo la Mapokezi Kijiji cha Munge Wilaya ya Siha tarehe 26/6/2023



Dkt. Haji Mnasi Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Siha akipokea Mwenge wa Uhuru katika eneo la Mapokezi katika Kijiji cha Munge Kata ya DonyoMurwak tarehe 26/6/2023.



Katibu Tawala Wilaya ya Siha Mhe. Jane Chalamila akipokea Mwenge wa Uhuru katika Kijiji cha Munge tarehe 26/6/2023. Mwenge wa Uhuru umepokelewa katika Wilaya ya Siha na kufungua, kutembelea na kuweka jiwe la msingi katika miradi 7 ya maendeleo.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Siha Mhe. Wilfred Mosi alivyoshiriki katika Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru ulipopokelewa katika Kijiji cha Munge tarehe 26/6/2023 .



Mkuu wa Wilaya Dkt Timbuka (kwanza kushoto mbele) akiwa na kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa ndugu Abdalla Shaib Kaim (pili kushoto mbele) wakikata utepe kabla ya kufanya ufunguzi rasmi wa shule ya Msingi na Awali Munge ambayo shule hii imefunguliwa rasmi tarehe 26/6/2023 na Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa.



Matukio mbalimbali yaliyoambatana na ufunguzi wa shule mpya ya Msingi Munge tarehe 26/6/2023



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha 5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677 Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz

MWENGE WA UHURU WATEMBELEA MRADI WA VIJANA KIJIKI CHA LAWATE TAREHE 26/6/2023



Mradi wa Vijana wa kuchomelea vyuma katika Kijiji cha Lawate Kata ya Kirua Wilayani Siha wamwagiwa sifa nyingi na Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa ndugu Abdalla Shaib Kaim na kiongozi huyo amesema kuwa mradi huu ni mfano bora wa kuigwa na vikundi vingine vya vijana hapa Nchini

MWENGE WA UHURU WAFUNGUA MADARASA MAWILI NA OFISI SHULE YA MSINGI KISHISHA KATA YA IVAENY



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa ndugu Abdalla Shaib Kaim (kulia) akifungua madarasa mawili na ofisi ya Walimu shule ya Msingi Kishisha tarehe 26/6/2023



Madarasa haya yamejengwa kwa shilingi milioni 47.7 ambapo milioni 45 ni kupitia Mapato ya ndani ya Halmashauri na nguvu na michango ya Wananchi ni shilingi milioni 2.7

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha 5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677 Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz

MRADI WA SHAMBA LA MACJARO PYRITA KILIMO CHA KARANGA MTI MACADAMIA NUTS



Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa ndugu Abdalla Shaib Kaim (katikati) tarehe 26/6/2023 akitembelea shambala kilimo cha karanga mti (Macadamia nuts) katika Kijiji cha Koboko Kusini Kata ya Nasai Wilaya ya Siha. Hadi mradi unatemelewa kiasi cha zaidi ya shilingi milioni 424.5 kimeshawekwezwa katika mradi huu mkubwa wa zao la biashara, Pia mradi huu unazalisha miche elfu 32 za Kahawa kwa lengo la kuboresha na kuinua kiwango cha uzalishaji wa zao la Kahawa.



MRADI WA UJENZI WA BARABARA YA LAMI SANYA JUU –NAIBILI-KIA



Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa ndugu Abdalla Shaib Kaim tarehe 26/6/2023 akiweka jiwe la msingi ujenzi wa barabara ya lami nyepesi yenye urefu wa kilomita moja kutoka Sanya Juu -Naibili – KIA. Ujenzi huu unatekelezwa kwa jumla ya shilingi milioni 480.2 kutoka Serikali Kuu na ajira za muda 182 zimepatikana katika kipindi cha utekelezaji wa mradi



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha 5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677 Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz

KLABU YA WAPINGA RUSHWA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NURU-MAKIWARU



Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa ndugu **Abdalla Shaib Kaim** akikabidhi klabu ya Wanafunzi Nuru Sekondari vitabu vya miongozo na elimu ya kuzuia na kupambana na Rushwa



MRADI WA UPANUZI WA ZAHANATI YA NAIBILI KATA YA MAKIWARU



Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa ndugu Abdalla Sahib Kaim akiweka jiwe la msingi upanuzi wa Zahanati ya Naibili tarehe 26/6/2023. Ujenzi huu unatekelezwa kwa shilingi milioni 271 kutoka Serikali Kuu kupitia mradi wa "Global Funds" na majengo matatu yanayojengwa ni jengo la Wagonjwa wa nje (OPD) ,Maabara pamoja na nyumba ya Mtumishi



Matukio mbalimbali hapo juu katika zoezi la kuweka jiwe la msingi upanuzi wa Zahanati ya Naibili Kaya ya Makiwaru

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha 5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677 Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz

MRADI WA UPANUZI WA SKIMU YA MAJI GARARAGUA



Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa ndugu Abdalla Saib Kaim alivyotembelea upanuzi wa skimu ya maji Gararagua tarehe 26/6/2023 . Fedha zinazotekeleza mradi huu ni jumla ya **shilingi milioni 693.75** fedha za uviko 19 pamoja na fedha za mfuko wa Maji wa Taifa



Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha 5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677 Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz

MAKABIDHIANO YA MWENGE WA UHURU TAREHE 27/6/2023




Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe.Dkt.Christopher Timbuka (kulia mbele) akimkabidhi Mwenge wa Uhuru Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu siku ya jumanne asubuhi tarehe 27/6/2023 katika uwanja wa CCM Sanya Juu.



Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya **Siha Dkt. Haji Mnasi** (aliyevaa trusksuti nyeusi) akiteta jambo na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu (pili kulia) wakati wa maandalizi ya kukabidhi Mwenge wa Uhuru katika uwanja wa CCM Sanya Juu Wilaya ya Siha **mapema tarehe 27/6/2023**.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha 5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677 Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz



**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA
YA SIHA LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA
MAWASILIANO SERIKALINI**

**Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha
5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha
Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677
Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz**

Tunapatikana

